LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# UTARATIBU WA UTOAJI WA MSAMAHA KWA WAFUNGWA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

HUMAN RIGHTS CENTRE NA HAKI ZA BINADAMU

# UTARATIBU WA UTOAJI WA MSAMAHA KWA WAFUNGWA

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

SHUKRANI ....................................................................................5
DIBAJI ........................................................................................5
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.............................................................................7
MAONO .......................................................................................8
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI ..................................................8
LENGO KUU ...............................................................................8
Utangulizi ..............................................................................9
Mfungwa ni nani? ..................................................................9
Aina za adhabu......................................................................10
Adhabu ya Kifungo Gerezani ..............................................11
Utumikiaji wa Kifungo Gerezani..........................................11
Msamaha kwa wafungwa ....................................................12
Sheria ya Msamaha kwa wafungwa..................................14
Bodi ya kitaifa ya msamaha kwa wafungwa................. 15
Bodi ya Mkoa ya Msamaha kwa wafungwa.................. 15
Akiwa nje kwa msamaha wa bodi; anatimiza masharti yaliyowekwa na bodi hiyo. .............................................17
Utaratibu wa kupeleka maombi ya msamaha kwenye bodi .............................................................18
Utaratibu wa kusikiliza maombi ya msamaha kwa wafungwa.............................................................................19
Hitimisho...................................................................................20

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani za dhati kwa wanasheria wetu Wakili Richard Manyota pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu hususani ofisi ya Arusha kwa kukiandaa kijitabu hiki.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi

kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo yapo Dar es Salaam. Pia Kituo kina ofisi nyingine Arusha na Dodoma

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

## Utangulizi

Utaratibu wa uendeshaji na usimamizi wa makosa ya jinai unasimamiwa na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20) kama ilivyorejewa mwaka 2019.

Sheria tajwa hapo juu, inatoa muongozo wa usimamizi na uendeshaji wa mashauri kuanzia pale mshukiwa wa kosa fulani anakamatwa, anafanyiwa upekuzi, anafikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa kosa la jinai na hatimaye mahakama inatoa maamuzi juu ya hatia au vinginevyo ya kosa aliloshtakiwa nalo.

## Mfungwa ni nani?

Baada ya mahakama kutoa maamuzi katika kesi ya jinai dhidi ya mshtakiwa na kama mahakama itajiridhisha pasi na shaka kuwa mshtakiwa ametenda kosa hilo aliloshtakiwa nalo, basi mahakama humtia mshtakiwa huyo hatiani na kumpa adhabu ya kifungo gerezani.

## Aina za adhabu

Kwa mujibu wa sheria ya kanuni ya adhabu, mahakama za Tanzania zinauwezo wa kutoa aina za adhabu zifuatazo dhidi ya mshtakiwa aliyethibitika kutenda kosa fulani;

a. Kifo;
b. Kifungo;
c. Kuchapwa viboko;
d. Kutoza faini;
e. Kunyang'anywa mali kama adhabu kwa kosa;
f. Kulipa fidia;
g. (Dhamana kwa kutunza amani na kuwa na tabia njema, au kwa kuhudhuria kupewa hukumu;
h. (Adhabu nyingineyo yoyote inayotolewa na Sheria ya Kanuni za adhabu au sheria nyingineyo yoyote.)

## Adhabu ya Kifungo Gerezani

Mahakama pamoja na mambo mengine kama ilivyokwishaelezwa hapo juu inaweza kutoa adhabu ya kumfunga gerezani mshtakiwa aliyethibitika pasina shaka kuwa ametenda kosa fulani la jinai. Adhabu hii ya kufungwa gerezani inategemea na kosa alilotiwa nalo hatiani mshtakiwa katika makosa na adhabu yanayoelezwa chini ya Sheria ya Kanuni za adhabu sura ya 16 marejeo ya mwaka 2019 na sheria nyingine zinazo ainisha jinai. Adhabu hii ya kifungo hutumikiwa gerezani kwa mujibu wa Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967.

## Utumikiaji wa Kifungo Gerezani

Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967 pamoja na mambo mengine imeweka bayana kuhusu mambo yafuatayo, yaani; ***Utawala wa Huduma za magereza, Mamlaka, wajibu na unafuu wa huduma za magereza, Mafao ya kustaafu yanayoweza kulipwa kwa maafisa wasio wa magereza, Afisa afya wa magereza,***

*Usimamizi wa magereza, Upokeaji wa wafungwa gerezani, Makosa kwa wafungwa, Unafuu kwa wafungwa na msamaha wa adhabu, Uondoaji wa wafungwa, Mafunzo na matibabu kwa wafungwa, Kizuizini na matibabu kwa mahabusu Pamoja na wafungwa wa madai, Uachiwaji kwa wafungwa na Makosa kwa wafungwa na adhabu kwa makosa hayo.*

Sheria hii ya magereza inaweka utaratibu wa namna ambayo kifungo cha gerezani kitatumikiwa na unafuu utakaopatikana pale ambapo mfungwa ataonyesha tabia njema wakati akiwa gerezani na au pale ambapo mfungwa atatenda kosa akiwa ndani ya gereza.

## Msamaha kwa wafungwa

Msamaha kwa wafungwa maana yake ni kuachiwa moja kwa moja au kwa muda kwa mfungwa kwa masharti ya kuwa mtu mwenye tabia njema katika jamii na au pamoja na masharti mengine mengi yatakayowekwa na chombo cha utoaji msamaha.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhiri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ana uwezo wa kutoa msamaha kwa wafungwa kwa mujibu wa sheria. Katiba inasomeka;

"Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika ibara hii, Rais anaweza kutenda lolote kati ya mambo yafuatayo:-

*(a) kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia mbele ya mahakama kwa kosa lolote, na anaweza kutoa msamaha huo ama bila ya masharti au kwa masharti, kwa mujibu wa sheria;*

*(b) kumwachilia kabisa au kwa muda maalum mtu yeyote aliyehukumuwa kuadhibiwa kwa ajili ya kosa lolote ili mtu huyo asitimize kabisa adhabu hiyo au asitimize adhabu hiyo wakati wa muda huo maalum;*

*(c) kuibadilisha adhabu yoyote aliyopewa mtu yeyote kwa kosa lolote iwe adhabu tahafifu;*

*(d) kufuta adhabu yote au sehemu ya adhabu yoyote*

*Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyopewa mtu yeyote kwa ajili ya kosa lolote au kufuta adhabu yote au sehemu ya adhabu ya kutoza, au kuhozi (au kuchukua) kitu*

*cha mtu mwenye hatia ambacho vinginevyo kingechukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano."*

## Sheria ya Msamaha kwa wafungwa

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Bunge limepewa mamlaka ya kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu utakaofuatwa na Rais katika utekelezaji wa madaraka yake ya kutoa msamaha kwa wafungwa.

Kwa mujibu wa sheria rais ana uwezo wa kuwaachia wafungwa wanaotumikia adhabu lakini zaidi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria Na. 400 ya mwaka 2002 ya Msamaha kwa wafungwa ambayo Pamoja na mambo mengine mengi ilianzisha bodi mbalimbali za utoaji wa misamaha kwa wafungwa kama inavyoelekezwa hapa chini;

## Bodi ya kitaifa ya msamaha kwa wafungwa

Kwa mujibu wa sheria ya bodi ya msamaha kwa wafungwa, sheria imeanzisha bodi ya msamaha kwa wafungwa kitaifa inayosimamiwa na Mwenyekiti wa bodi ambaye anachaguliwa na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania. Wajumbe wengine wa bodi hii ni pamoja na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali au mwakilishi wake, Afisa Muuguzi mkuu kutoka wizara ya Afya, Kamishna wa ustawi wa jamii, Afisa mwandamizi kutoka ofisi ya Rais pamoja na wajumbe wawili wenye maadili mazuri katika jamii watakaoteuliwa na waziri anayehusika na maswala ya magereza.

## Bodi ya Mkoa ya Msamaha kwa wafungwa

Bodi hii ya mkoa pia huanzishwa na sheria ya bodi ya msamaha kwa wafungwa. Bodi hii inaongozwa na Mwenyekiti ambaye

uteuliwa na waziri anayehusika na maswala ya magereza, mwanasheria mkuu wa serikali wa mkoa husika au kanda, Afisa muuguzi mkuu wa mkoa husika, Afisa mwandamizi wa ustawi wa jamii toka ofisi ya ustawi wa jamii ya mkoa husika, Afisa mwandamizi mwakilishi kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa husika pamoja na wajumbe wengine wanne wenye maadili mazuri katika jamii watakao chaguliwa na waziri anayehusika na masuala ya magereza.
Vigezo vya kupata msamaha kwa wafungwa

Sheria imeweka vigezo maalum vitakavyo angaliwa na bodi husika kabla ya kukubali ombi la mfungwa kupewa msamaha navyo ni;

a. *Asiwe anatumikia adhabu ya kifungo cha Maisha gerezani;*
b. *Asiwe anatumikia adhabu ya kifungo kutokana na makosa ya wizi wa kutumia silaha (armed robbery), kujihusisha na madawa hatarishi (dangerous drugs) na au unajisi (defilement)*
c. *Adhabu yake isiwe imekwisha kupunguzwa.*

d. *Awe ametumikia adhabu kwa miaka minne au moja ya tatu ya adhabu husika; yoyote itakayo kuwa nyingi.*

e. *Amekuwa akionyesha tabia njema wakati wote akiwa anatumikia adhabu yake kabla ya kwenda kwenye bodi ya msamaha.*

## Akiwa nje kwa msamaha wa bodi; anatimiza masharti yaliyowekwa na bodi hiyo.

### Kushindwa kutimiza masharti ya msamaha

Mfungwa anapopata msahama wa bodi anapaswa kutimiza masharti ya msamaha yaliyowekwa na bodi husika. Kushindwa kutimiza masharti hayo kuna madhara kama ifuatavyo;

a. *Kukamatwa na kushtakiwa kwa kosa la kuvunja masharti ya msamaha.*

b. *Kutiwa hatiani; kutumikia adhabu ambayo alipewa msamaha;*

c. *Kutumikia adhabu ya kuvunja masharti ya msamaha wa bodi.*

## Utaratibu wa kupeleka maombi ya msamaha kwenye bodi

Kwa mujibu wa sheria, Afisa mkuu mwangalizi wa gereza akiona mfungwa ameweza kukidhi vigezo vya kupewa msamaha kwa mujibu wa sheria, anaweza kushauri bodi ya mkoa ya msamaha kwa wafungwa kumsamehe mfungwa huyo.

Mfungwa anaweza kupeleka maombi yake mwenyewe moja kwa moja katika bodi ya msamaha kwa wafungwa kama anaona kuwa amekidhi vigezo vya kisheria vilivyoainishwa hapo juu. Lakini pia kama afisa mkuu mwangalizi wa gereza alishauri mfungwa fulani kuachiwa kwa msamaha, mfungwa huyo anaweza pia pamoja na ushauri wa afisa mkuu mwangalizi wa gereza kupeleka maombi yake katika bodi ya msamaha kwa wafungwa kwa ajili ya kuomba msamaha.

## Utaratibu wa kusikiliza maombi ya msamaha kwa wafungwa

Mara tu baada ya bodi ya mkoa ya msamaha kwa wafungwa kupokea maombi husika kutoka kwa mfungwa au ushauri kutoka kwa Afisa mkuu mwangalizi wa gereza, itachukua maombi hayo na kuyapitia, kuchambua na kuyatathmini ili kujiridhisha kama mfungwa huyo amekidhi vigezo na kisha watapeleka majibu yao katika bodi ya taifa ya msamaha kwa wafungwa.

Mara baada ya bodi ya taifa ya msamaha kwa wafungwa kupembua kiyakinifu juu ya maombi yaliyoletwa na mfungwa husika, itapeleka mapendekezo kwa waziri anayehusika na masuala ya magereza kwa hatua zaidi.

Mara baada ya waziri husika kupitia mapendekezo ya bodi ya taifa ya msamaha kwa wafungwa pamoja na ripoti mbalimbali za mfungwa husika, anaweza kukubali msamaha

huo au kukataa maombi hayo ya msamaha. Isipokuwa, kama waziri atakataa maombi ya msamaha husika, anapaswa kisheria kutoa sababu za kukataa huko kimaandishi.

## Hitimisho

Kila mfungwa anayekidhi masharti ya kuomba msamaha kwa mujibu wa sheria ana uwezo wa kupeleka maombi yake katika bodi husika. Ikumbukwe sekretarieti ya bodi ya mkoa ya msamaha kwa wafungwa ipo katika ofisi za magereza za mkoa husika na sekretarieti ya bodi ya taifa ya msamaha kwa wafungwa ipo katika ofisi za Kamishna Mkuu wa Magereza.

Sweden Sverige

Norwegian Embassy

FORD FOUNDATION

Irish Aid
Rialtas na hÉireann
Government of Ireland

Ministry for Foreign Affairs of Finland


**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV